

SOMO LA 3

BIBLIA: JINSI ILIVYOTUJIA-Sehemu ya 2

MISWADA ILIYO NA AGANO ZOTE MBILI

TOLEO LA ASHURU lilikuwa ni tafsiri ya wale Wakristo wa mwanzo waliokuwa wakikaa maeneo ya milima ya Ashuru.

Hili lilikuwa toleo la awali la Agano Jipya, iliyotafsiriwa mnamo mwaka wa 150 baada ya kuwepo Kristo, karibu wakati mmoja na maandishi ya mitume.

Ilikuwa na Agano La Kale na Jipya, ikiwa imetafsiriwa kutoka kwa kazi ya Kiyunani ya wazee sabini. Nakala ya toleo hili yanapatikana hivi leo, yamehifadhiwa mjini Leningrad katika nchi ya Urusi, pia katika jumba la utawa liliopo Sinai. Toleo hili, kama ilivyo toleo hili la wazee sabini, ni kazi muhimu sana kwa watafsiri na wanafunzi wa Biblia.

MATOLEO YA KILATINI yaliwafaa sana wakazi wa Afrika Kaskazini, hasa wale wa Carthage ambao lugha yao kuu ilikuwa Kilatini. Mswada huu ulijulikana kama Kilatini Cha Afrika, iliyoandikwa mwaka wa 300 baada ya majilio ya Kristo. Matoleo mengine mengi ya Kilatini yalizidi kutolewa wakati huu ambapo Kilatini kilitumika zaidi kulilo Kiyunani. Lakini pakatokea shida; matoleo mengi haya yalihitilifiana na kukakuwepo ainaaina na makossa dhahiri katika nakala hizi na ikalazimu kududusa kazi hiyo. Kazi ya urekebishaji ikamlelea mwanazuoni makini sana wa karne ya tatu aitwae Yerome.

Alitumia miswada ya Kiebrania ya Agano La Kale katika kazi yake ya utafsiri, Toleo La Wazee Sabini, na miswada ya Ashuru ya Agano La Kale.

Agano Jipya ni kazi iliyopitiwa ya miswada ya awali ya Kilatini, kwa msaada wa mswada wa Kiyunani na Kiashuru. Kazi yake ilikamilika mnamo mwaka wa 386 wa Bwana Wetu, na inajulikana maarufu kama **VALIGETI YA KILATINI**. Nakala 30,000 hivi zilichapishwa na kusambazwa. Kwa miaka mingi toleo hili lilichukuliwa (na bado lachukuliwa na Kanisa La Kirumi) kama kitabu sahihi, na imekuwa na mvuto mkuu kwa matoleo mengi ya kisasa kama tutakavyoona.

TOLEO LA SINAI – yaitwa hivyo kwa sababu ya kugunduliwa katika makao ya watawa Sinai. Iliandikwa mnamo mwaka wa 300, na ni Agano La Kale na Jipya katika lugha ya Kiyunani. Iliwapotelea walimwengu mwanzoni hadi ilipofichuliwa Sinai mwaka wa 1853. Ilipelekwa Leningrad mwanzo, kisha ikanunuliwa na makavazi ya Uingereza mwaka wa 1933.

TOLEO LA VATIKAN – Nukuu ya asili ilitokana na Toleo La Wazee Sabini na miswada ya Kiyunani ya Agano Jipya ya mwaka wa 370, ambayo ilijumuisha Biblia nzima ya Kiyunani, ingawa sehemu zingine hazipatikani kwa sasa kwa sababu ya ukale. Mswada huu unapatikana

katika Maktaba ya Vatikan, ingawa haijulikani hasa lini au vipi ilikuja hapo Vatikan. Haikutolewa kwa watafsiri hadi mwaka wa 1867.

MSWADA WA ALEKSANDARIA – Mswada wa Kiyunani wa Biblia nzima ulioandikwa Mwaka wa Masihi 400., sasa ukiwa umepungua sehemu fulani. Ulipeanwa kwa Uingereza mwaka wa 1624 na sasa wapatikana katika Makavazi ya Uingereza. Ni ushahidi muhimu kwa miswada ya wazee sabini na Agano Jipya kwa Kiyunani.

Wakati nakala hizi zote zilipokuwa zikiandikwa, mabadiliko makubwa tena ya kasi yalikuwa yaendelea katika ulimwengu wa uandishi na dini.

Lugha iliyokuwa yachukua nafasi ya mbele ni Kilatini. Siku zilipozidi kusonga ndipo Kiyunanani na Kiebrania zilivyozidi kusahaulika hata na wasomi wa wakati huo. Hii ndio sababu miswada kama hii ambayo tumeipitia iliweza kutupwa katika kapu la sahu mara ilipoandikwa.

VALIGETI YA KILATINI ilipandishwa hadhi na Kanisa La Roma kuwa toleo la pekee la kweli la Biblia. Walisahau kuwa ilikuwa tu kazi ya utafsiri kwa miswada hii ya Kiebrania na Kiyunani. Walisema hivi kuhusu “Vulgate,” “Ni toleo la Kanisa, katika lugha yake yenyewe (Kilatini); kwa nini ikubali miswada ya Kiyunani na Kiebrania ambayo kwa miaka mingi imekuwa ni ya Wayahudi wasioamini na Wayunani wapotovu? Mtazamo huu ulitayarisha uwanja wa fujo wa kukabiliana na yeyote atakayejaribu kutafsiri maandiko kwa lugha za wenyeji kwa kuwavunja na kuwatesa. Walijiona kama wahifadhi wakubwa wa Biblia na wakajitahidi kuwazuia watu yakhe kuifikia. Walifaulu kuwazuia watu kuifikia miswada ya Valigeti; lakini kwa kuwa nakala za mwanzo zilikuwa nyingi (30,000), wengi waliweza kusoma Biblia hii ingawa umaarufu wake ukawa wapungua katika karne zilizofuata kutokana na kubadilika kwa umaarufu wa lugha. Kwa namna fulani “kanisa” ikapata afueni pale ambapo lugha ya Kilatini ikawa yatumiwa na watu wachache, hivyo watu wengi wakakosa uwezo wa kujisomea Biblia kwa lugha hiyo.

TOLEO LA ANGLO-SAKSONI-

Nakala chache zilitokea karne ya kenda Mwaka wa Masihi. Hazikunoga kwani ni nakala chache zilitolewa, na lugha hii ilikuwa haijashika kasi, ikawa yapitia mabadiliko mengi.

Matoleo haya yalikuwa ni tafsiri ya moja kwa moja toka kwa valigeti ya Kilatini hadi lugha ya Anglo-Saksoni. Nakala zilizotolewa baadaye zikawa zafuata mkondo wa kurekebishwa pindi lugha inavyobadilika, hivyo mabadiliko na masahihisho mengi yalifanyika katika kipindi hiki cha historia.

BIBLIA YA WYCLIFFE-

Mwaka wa 1350 hivi, Mwingereza fulani ajulikanaye kama John Wycliffe alitafsiri Valigeti ya Kilatini kwa lugha ya Kiingereza. Kwa mara ya kwanza watu wa Uingereza walipata Biblia ambayo wangeweza kuisoma na kuielewa katika lugha yao wenyewe. Hata hivyo, ufanikishaji

huu uliweza kuibua ghadhabu na hasira ya Kanisa La Roma, ambalo lilimwona Wycliffe, kwa jicho la askofu kama “Huyo fedhuli msumbufu, mwana wa joka la zamani, mtangulizi wa mpinga kristo, ambaye amekamilisha uovu wake kwa kubuni tafsiri mpya ya Maandiko.” Kabla hawajachukua hatua kali ya kisasi chao kiovu, alijifia kifo cha kawaida katika hali tulivu na ya amani. Lakini moto wa hasira ya makasisi waliojaa ghadhabu ilipulizwa na wengi wa wafuasi wa Wycliffe waliadhibiwa kwa kuuawa. Wasomaji wa Biblia walichomwa wangali hai wakiwa wamefungiwa nakala za Biblia zao shingoni. Wazazi waliangamizwa kwa kuwafunza wanao sala ya Bwana na Amri Kumi kwa Kiingereza; mabwana na mabibi walilazimishwa kutoa ushahidi dhidi yao kwa wao; watoto walitumiwa kuuwasha moto wa kuwateketeza wazazi wao hali wenyewe wakiangalia wanavyochomeka. Waliwawinda wale waliokuwa na nakala za Biblia ya Wycliffe kama mtu awindavyo mnyama. Wakati huo huo haya yakiendelea, mambo mengi yalikuwa yanaendelea yaliyokuwa yanaelekeza na kumaliza vita vya Kanisa hili. Kwanza, Biblia ya Wycliffe ndiyo iliyokuwa ya mwisho kuandikwa kwa mkono, punde pakatokea ubunifu wa vyombo vya uchapishaji. Pili, pakatokea haja ya kupendelea lugha za kiyunani na Kiebrania na hivyo mwamko mpya katika kazi ya utafsiri. Nakala mpya za miswada ya Kiebrania na Kiyunani zilikuwa zimetolewa karne ya 12 wakati maendeleo ya usomi na wanazuo ulipochanganyika na marekebisho ya Kanisa, pakatokea kipindi kilichowaleta akina Erasmus na WilliamTydale

KUCHAPISHWA KWA BIBLIA KWA MASHINE YA UCHAPISHAJI

Erasmus alikuwa mtaalamu wa lugha ya Kiyunani, na kazi yake iliegemea sana upande wa Agano Jipya. Hili toleo la Agano Jipya lilikuwa mwanzo kuchapishwa kwa mashine. Lilichapishwa kwa Kiyunani kutoka kwa miswada ya Kiyunani ya karne ya 10 na 12. Mwanachuo mwingine, XIMENES, alikuwa na Agano Jipya iliyokuwa tayari kuchapishwa. Mchapishaji wa Erasmus alimshinikiza achapishe kazi yake mwanzo. Shinikizo hili halikuwa la kusaidia usahihi. Erasmus alifaulu kuchapisha maandishi yake mwanzo, lakini baadaye alikiri kuwa usahihi wa makala ulitatizika kiasi kwa sehemu fulani. Kwa bahati nzuri, makosa hayo ni dhahiri sana na ni rahisi kutambuliwa na msomi mzuri.

Mfano wa mizani ni kifungu katika 1 Yohana 5: 6,7 Toleo la King James. Ilitafsiriwa kutoka kwa toleo la Valigeti na kuingizwa kwa udanganyifu katika mojawapo ya miswada ya Kiyunani ya Erasmus. Aliuona huo udanganyifu, lakini kwa haraka aliyokuwa nayo na shinikizo la kuchapisha aliamua kujitia hamnazo. Kifungu hiki hakipatikani katika mswada mwingine wowote, na toleo la Marudio limeacha kukitumia kifungu hiki.

WILLIAM TYNDALE

William Tyndale aliishi wakati mmoja na Erasmus. Wote waliishi kipindi chicho hicho cha mwaka wa 1500 Baada ya Masihi. Tyndale alikuwa jasiri na mwenye ujuzi wa ajabu wa lugha ya Kiyunani na Kiebrania. Toleo lake la Biblia lilikuwa ni tafsiri ya moja kwa moja kutoka kwa kazi asili ya Kiibrania na Kiyunani, na ushawishi fulani kutoka Valigeti ya Kilatini na kazi ya Erasmus. Maelfu ya nakala ya Biblia iliyokamilika katika lugha ya Kiingereza ilichapishwa na

kuwafikia wenzake waliokuwa wanasubiri kwa hamu na ghamu kupokea. Mara maisha yake yakawa hatarini Uingereza na akatorokea Ujerumani. Uchapishaji kwa mashine uliendelea na Biblia zikawa zasafirishwa kimagendo kwa marobota ya nguo na magunia ya unga. Mafanikio yalikuwa ya ajabu, kwani ni Biblia nyingi zilizofika na baadaye kuangamizwa kwa kuchomwa. Na hata huko Ujerumani, mtu alimsaliti. Akapelekwa katika gereza ya kuhuzunisha karibu na mji wa Brussels, mahali ambapo maisha yake yalikuwa mikononi mwa watu wasio na nehema wala huruma, baadaye alichukuliwa na kufungwa kwenye mti ambapo walimnyonga na kumchoma moto. Lakini kazi yake, ikaendelea.

TOLEO LA MFALME JAMES – KING JAMES VERSION

Wakati wa matokeo ya kifo cha Tyndale, Henry VIII aligombana na Papa wa Roma, na matokeo ya ugomvi huu ukazalisha Kanisa la Uingereza. Henry pamoja na Kanisa la Uingereza, wakawa wanapendelea watu wao kuwa na Biblia zao. Maaskofu wa Kiingereza walikuwa wamekasirishwa na unyanyapaa wa jina la Tyndale, na huko kazi yake haikuungwa mkono nao. Biblia zingine zilizofuata, zilikuwa ni kama matoleo ya Biblia za Tyndale. Halafu, mwaka wa 1611, Mfalme James I alitoa amri ambayo ilisababisha kutafsiriwa na kuchapishwa kwa King James Version – Toleo la Mfalme James. Iliyotofautiana kidogo sana na Biblia ya Tyndale, msingi wa chanzo chake ukiwa ni uleule – miswada ya Kiebrania na Kiyunani ya Karne ya 12 Baada ya Masihi; na kwa upande mwingine kuchangiwa na Valigeti ya Kilatini. Takribani 80% ya Agano la Kale na 90% ya Agano Jipya yaonekana imehamishwa moja kwa moja kutoka katika Biblia ya Tyndale.

Tafsiri inayojulikana kama “King James Version” – Toleo la James – imeathiri pakubwa maisha na fasihi ya ustaarabu wa watu wa Ulaya. Ni zaidi ya Karne 3 tangu nakala ya kwanza ichapishwe. Ni Toleo ambalo lakubalika na wengi, ingawa, kwa kuwa lugha ya Kiingereza yapitia mageuzi mengi, maneno mengi yaliyotumika yamebadilisha maana au sasa hayatumiki tena kwani ni kuukuu.

TOLEO JIPYA – REVISED VERSION

Kugunduliwa kwa miswada ya kale baada ya kuchapishwa kwa Toleo la mfalme James – kama vile mswada mpya wa Samaria, mswada wa Vatikan, mswada ya Aleksandria, na mingineyo – ilifanya Toleo Jipya liandaliwe na kazi hiyo ilianza mwaka wa 1870 na kukamilika mwaka wa 1885. Marudio mengine yalifanywa baadaye na TOLEO JIPYA SANIFU – REVISED STANDARD VERSION likapatikana. Kwa upande wa Kiingereza, TOLEO LA MFALME JAMES na Toleo Jipya Sanifu tuna neno asili la Mungu katika lugha moja. Tutaeleza thamani ya kuwa na matoleo haya mawili baadaye.

UGUNDUZI WA HIVI KARIBUNI

Katika miaka ya 1940 ugunduzi mkuu ulifanyika. Miswada ya Misri tuliopitia katika somo la 2 iligunduliwa kutoka ardhini mwaka wa 1941, na imekuwa ya msaada mkubwa katika kuhakikisha usahihi wa matoleo ya kisasa ya Agano Jipya. Ugunduzi wa vitabu vilivyopatikana katika Bahari ya chumvi katika mwaka wa 1947 vimesaidia sana kwa upande wa Agano La Kale. Viko katika lugha ya Kiebrania na ni vya zaidi ya miaka 2000 – kufikia kuja kwa Yesu au kabla ya kuja kwake. Ni kama za wakati mmoja na Biblia ya Kiyunani ya wazee Sabini. Viliinakiliwa na watu wa Qumran – kundi la kidini la wakati huo. Tena, kama ilivyo miswada wa Misri, inasaidia katika kuangalia usahihi wa Biblia zetu. Kazi tele inaendelea kwa ugunduzi huu na muda unavyosonga ndivyo linavyoweza kuwa na tafsiri kamili katika lugha ya Kiingereza na hata Kiswahili.

Kuna jambo la kuangalia kwa makini hapa, miswada ya Misri na ile ya Bahari ya Chumvi zinaunga mkono tafsiri zilizopo kwa sasa, hasa Toleo La Mfalme James na Toleo Jipya Sanifu. Watafsiri na waliofanya kazi ya kunukuu kwa karne kadhaa wanafaa pongezi tele, kwani kwa vitabu vile vya Bahari ya Chumvi tuna hazina ya miswada ambayo ni ya zaidi ya miaka 1000 kuliko ile iliyokuwepo lakini tofauti ni kidogo sana. Ama tuseme, kuna uwezekano wa nguvu za kuwaongoza waliofanya kazi ya utafsiri na kunukuu maandiko iliyo na nguvu na thabiti na sahihi kuliko matakwa na mapenzi ya mwanadamu. Inatuzungumzia juu ya nguvu inayofanya kazi kwa njia ya kawaida lakini hatimaye inatimiza kile ambacho kilitarajiwa kiwe kwa ubunifu tangu hapo.

WAZO LA BAADAYE

Umewahi kuwazia ni nini hasa Mungu anataka kutoka kwako? Na katika masomo haya yote , kuajabia – “Nahusikaje katika mambo haya?” Biblia yatuambia wazi alichotoa Mungu, na kinachoweza kutuhusisha na kutufaa...

Mpango wa Mungu ni kuujaza ulimwengu huu kwa utukufu wake. Ni kuijaza dunia na watu walio sehemu yake. Kinachohitajika kutoka kwetu ni kuanza kumtumikia sasa. Huu ndio wakati wa kuwa mwanawe wa kiume au kike. Twafanya hivi kwa kumwamini, na kuyaamini Anayosema na kumwamini Mwanawe Yesu. Halafu yafaa kutubu dhambi zetu – tukiri kutenda dhambi halafu tubatizwe tukisha amini mambo yanayohusu Ufalme wa Mungu na Jina La Yesu Kristo. Halafu yafaa tuishi maisha yanayomweka Mungu mwanzo – tuheshimu amri zake – amri kuu ikiwa ni upendo. Kuna njia za upendo, wema, furaha na haki. Zinahusiana na kuwasaidia wengine na kusaidiana. Wazia hili. Tafadhali tafakari haya unapoendelea kuyapitia masomo haya.

Waweza kupata mpango wa kusoma Biblia kila siku kutoka hapa:

<http://www.keytobibletruth.com>

tafadhali weka maswali haya pamoja kwa njia ya barua pepe kisha utume majibu yako kwangu:

bereanafric@gmail.com

MASWALI KWA SOMO LA 3

1. Toleo la Siria lina umuhimu gani?
2. Nini kilitoa msukumo wa kuandika Valigeti ya Kilatini?
3. Je, Sera ya Kanisa la Roma kuhusu Valigeti ya kilatini inakwenda sambamba na ukweli wa historia?
4. Je, Valigeti ya kilatini iliweza kuwafikia watu kwa urahisi?
5. Nini ilifanya Biblia ya Wycliffe iwe tofauti na zote zilizotangulia?
6. Ni nini kilichotokea kwa wale waliomiliki Biblia ya Wycliffe?
7. Ni Biblia gani ya mwanzo iliyochapishwa kwa mashine.
8. Biblia hii ilikuwa na udhaifu gani?
9. Vitabu vyanzo vya Biblia ya Tyndale vilikuwa gani?
10. Wakuu walichukuliaje kuchapishwa kwa Biblia ya Tyndale?
11. Watu yakhe walichukuliaje kuchapishwa kwa Biblia ya Tyndale?
12. Ni hali gani iliyomkasirisha Mfalme James I kutoa amri ya kutafsiri na kuchapishwa kwa Toleo la Mfalme James?
13. Vitabu vyanzo vipi vilitumiwa katika kuchapisha Toleo La Mfalme James.
14. Je, Sehemu kubwa ya Toleo La James lilitafsiriwa au ni kuhamishwa tu?
15. Kwa nini ni muhimu kujua tofauti hii?
16. Ni nini kilitoa msukumo kwa kuandikwa kwa Toleo Jipya?
17. Je, Matoleo ya Mfalme James na Toleo Jipya hufikiriwa kuwa ndio upitishaji wa kuaminika wa neno la asili la Mungu?
18. Kwa nini miswada ya Misri na vitabu vya Bahari ya Chumvi ni muhimu?